JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# TRC yaandika historia mpya Afrika

- **Tanzania, Burundi kutimiza ndoto za Wabelgiji, Wajerumani za tangu karne ya 19**
- **Kujenga reli ya kisasa ya kwanza kuunganisha mataifa miaka 50 baada ya TAZARA**
- **DG TRC: Mradi wa SGR Tanzania haujasimama, utakamilika kabla ya mwaka 2030**

**MUSONGATI**

NA MWANDISHI **WETU**

Agosti 16, 2025 itabaki kwenye kumbukumbu kwa mataifa mawili ya Afrika; Tanzania na Burundi, kama siku rasmi ya kuanza kwa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Ni ujenzi utakaobadili kwa kiwango kikubwa sekta ya usafiri na usafirishaji ukanda wa Afrika Mashariki, ikijengwa kutoka Uvinza nchini Tanzania hadi Musongati, Burundi, kipande cha takriban kilomita 300.

Kwa Tanzania hii itakuwa reli ya tatu inayoiunganisha Tanzania na nchi jirani; ikitanguliwa na reli ya Moshi hadi Voi nchini Kenya, kisha Reli ya TAZARA kutoka Dar es Salaam hadi Kapirimposhi, Zambia.

Lakini kwa Burundi SGR ya Uvinza – Musongati itakuwa reli ya kwanza tangu kuumbwa kwa ulimwengu, ikitarajiwa kuwanufaisha Warundi kwa kuliunganisha taifa lao na Bandari ya Dar es Salaam; lango muhimu la biashara na uchumi.

Reli hii inajengwa kwa usimamizi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) chini ya



Rais Samia Suluhu Hassan

Mkurugenzi Mkuu, Mhandisi Machibya Shiwa.

Mwenyeji katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la SGR ya Uvinza – Musongati alikuwa Rais wa Burundi, Jenerali Evariste Ndayishimiye huku Rais Samia Suluhu Hassan akiwakilishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Jenerali Ndayishimiye anaamini kuanza kwa ujenzi wa SGR kutakuwa jawabu la shauku ya muda mrefu kwa Warundi na hata Watanzania kama si wananchi wa eneo zima la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Leo ni siku ya furaha sana kwetu. Tumepata jawabu la ndoto za tangu enzi na enzi. Wazo la mradi huu lilianzishwa na Wabelgiji kisha wakaja Wajerumani, lakini wote wakashindwa. Leo hii Tanzania na Burundi tumeweza," anasema Rais Ndayishimiye.

Anasema Burundi Ilikuwa na ndoto ya kuwa na usafiri wa reli utakaokuza uchumi wa taifa hilo ambalo asilimia 100 ya shehena zake zinazosafirishwa kwa maji hupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Jenerali Ndayishimiye aliyewahi kuitisha kongamano la wawekezaji wa ndani na nje ya Burundi kujadili namna wanavyoweza kunufaika na uchimbaji madini, anasema hakukupatikana matokeo chanya kutokana na changamoto ya usafiri na usafirishaji.

"Wawekezaji wengi walitamani kuanza kuwekeza mara moja, lakini wakaniuliza; 'tukianza kuchimba Nickel, tutaisafirishaje?'" anasema, akiutaja ujio wa reli kama hatua madhubuti ya kuwakwamua kiuchumi wananchi wa



Vifaa vya ujenzi wa SGR ya Uvinza - Msongati (kushoto) vikiwa tayari kuanza kazi. TRC inasimamia ujenzi wa reli hiyo ya kwanza ya SGR kuvuka mipaka ya kimataifa Afrika Msharìki na Kati

Burundi.

Anasema changamoto hiyo iliwafanya yeye na viongozi wenzake kukaa chini na kutafuta suluhisho na kuishukuru Tanzania kukubali kuungana na Burundi kufanikisha kuanza kwa mradi huo muhimu.

Rais Ndayishimiye, anayezungumza Kiswahili kwa ufasaha, amempongeza Dk. Samia kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na maendeleo hivyo kuifanya Tanzania ipige hatua kubwa mbele.

"Tanzania siku zote imekuwa baraka kwetu," anasema akitaja maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam anayoyajua ingawa sasa akifika anaweza kupotea kutokana na maendeleo makubwa yaliyopo.

**Waziri Mkuu azungumza**

Akizungumza kabla ya Jenerali Ndayishimiye, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anasema uwekaji jiwe la msingi ni alama ya safari ya maendeleo kwa wananchi wa EAC.

"Tunawahakikishia Watanzania na Warundi kwamba ujenzi huo utaanza katika muda uliopangwa na kumalizika kwa wakati.

"Hii ni kutokana na viongozi wetu; Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Jenerali Ndayashimiye kuwa na dhamira njema kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati na kuwa na mafanikio," anasema Majaliwa.

SGR ya Uvinza – Musongati itakayokuwa na urefu wa kilomita 240, itakuwa ya kwanza kuunganisha mataifa mawili ya Afrika Mashariki, akitaka kila mwananchi kujivunia dira na maono makubwa ya viongozi wakuu wa Burundi na Tanzania.

"Itakapokamilika itaunganisha masoko na kuendeleza biashara baina ya Tanzania na Burundi; itafungua fursa kwa wananchi watakaokuwa wakisafiri kwa siku moja kutoka hapa (Musongati) hadi Dar es Salaam," anasema.

Kwa sasa shehena ya mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Bujumbura, Burundi hutumia saa 96; muda utakaopungua hadi saa 20 tu reli itakapoanza kufanya kazi.

Jumla ya dola za Marekani bilioni 2.154 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa kipande cha Uvinza – Musongati utakaokamilika ndani ya miaka mitano huku kukiwa na mwaka mmoja wa matazamio.

Kauli ya Majaliwa inaungwa mkono na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, akiongeza kwamba utekelezaji wa mradi unakwenda sambamba na Ajenda 63 ya Umoja wa Afrika (AU) inayotaka Bara la Afrika liunganishwe kwa mtandao wa reli ya kisasa.

Anasema reli hiyo itakapokamilika, itapunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kati ya Dar er Salaam na Bujumbura, Burundi.

"Kwa sasa gharama za kusafirisha kontena moja la futi 20 ni dola za Marekani 3,800; lakini reli itakapokamilika, itashuka hadi dola za Marekani 2,000. Haya ni mageuzi makubwa katika sekta ya usafirishaji," anasema Profesa Mbarawa.

Anataja faida nyingine kuwa ni kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja. "Hivi sasa mzigo unaosafirishwa kwa lori moja ni tani 30, lakini reli ikianza kazi, tutasafirisha tani 3,000 kwa wakati mmoja na kufika ndani ya siku moja," anasema Profesa Mbarawa.

Baadaye, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Mhandisi Machibya Shiwa, akapata nafasi ya kutoa maelezo ya kitaalamu kuhusu utekelezaji na ujenzi wa mradi huu kwa Jenerali Ndayishimiye na Kassim Majaliwa.

Mhandisi Machibya akawaongoza viongozi hao hatua moja baada ya nyingine ya ujenzi, akiwaonyesha kwa ushahidi mwonekano wa SGR ya Uvinza – Musongati itakavyokuwa itakapomalizika.

Siku kadhaa kabla ya kwenda Burundi kwenye hafla hiyo, Mhandisi Machibya alizungumzia ujenzi wa mradi wa SGR kwa ujumla, akitoa rai kwa Watanzania kupuuza madai kwamba mradi umesimama.

Shirika la Reli nchini (TRC) limewataka wananchi kupuuza taarifa potofu zinazosambazwa na baadhi ya



Wamamchi wa Tanzania na Burundi wakishiriki uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR ya Uvinza - Musungati

watu wanaodai kuwa mradi wa SGR umesimama.

Akizungumza kwenye Banda la TRC wakati wa Maonyesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam, Mhandisi Machibya Shiwa, amesema tayari shirika limepata makandarasi wa ujenzi wa vipande vya reli hadi Mwanza na kutoka Tabora hadi Kigoma, ikijumuisha kipande cha Uvinza mpaka Musongati, Burundi.

Amesema mradi huo utakamilika kabla ya mwaka 2030, kulingana na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa fedha za kutosha zipo.

**Historia**

Januari 22, 2022, Tanzania na Burundi ziliingia makubaliano ya ujenzi wa reli hii, ikiwa ni mwendelezo wa ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa kutoka Tabora hadi Uvinza.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Mhandisi Machibya Shiwa

Sekta ya uchukuzi nchini imekuwa na mafanikio makubwa tangu Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dk. Samia iingie madarakani, lengo likiwa ni kukuza uchumi kupitia sekta ya usafiri na usafirishaji kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020 - 2025.

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa thamani ya dola za Marekani bilioni 2.54.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Katibu Mtendaji wa 'Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency (CCTTFA)', mdau mkubwa wa usafirishaji wa shehena ushoroba wa kati, Wakili Okandju Okonge, amesema reli hii ni utekelezaji wa vipaumbele vya PIDA chini ya Mtandao wa Reli za Kasi za Bara la Afrika (AIHSRN).

Ameelezea mchango wa CCTTFA katika maandalizi ya mradi, ikiwa ni pamoja na kuratibu mikataba ya pande tatu na ya nchi mbili, kuhamasisha rasilimali kutoka kwa serikali na wadau wa maendeleo, kuratibu viwango vya kiufundi vya usafirishaji wa kuvuka mipaka, na kuwashirikisha wadau kuhakikisha manufaa jumuishi na umiliki endelevu wa mradi.

Wakili Okandju Okonge ametoa wito wa kuendeleza juhudi katika hatua zinazofuata za mtandao huu wa reli ya kikanda, hasa sehemu ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

"Utafiti wa awali wa uwezekano wa mradi wa reli kutoka Gitega – Bujumbura/Uvira – Kindu unaendelea, ukiwa ni hatua muhimu kuelekea kuimarisha uhusiano wa usafirishaji na biashara katika kanda," amesema Wakili Okandju Okonge.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya China Railway Group Limited, kiongozi wa muungano wa kampuni zinazojenga reli hiyo ya kuvuka mpaka inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2030.



Rais wa Burundi, Jenerali Ndayashimiye akiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, viongozi na wadau wengine wa sekta ya usafirishaji

CamScanner

# SGR Uvinza-Musongati, funguo muhimu milango mipya ya uchumi

**Na Shakila Mtambo**

AGOSTI 16, 2025 serikali ya Tanzania na ya Burundi ziliweka jiwe la msingi kuashiria kuanza kwa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kipande cha saba na nane kutoka Uvinza mkoani Kigoma hadi Musongati Burundi.

Uzinduzi wa mradi huo wa kihistoria kwa nchi hizo ulishuhudiwa na Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye na viongozi wengine wa nchi hiyo, kwa upande wa Tanzania Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Reli hiyo itakuwa na urefu wa kilometa 300, kilometa 240 za njia kuu na kilometa 60 za njia za kupishania na unatarajiwa kuwa na stesheni za kupakia abiria na mizigo.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema kipande cha saba kutoka Uvinza-Malagarasi kitakuwa na urefu wa kilometa 190, kilometa 156 njia kuu na kilometa 34 njia za kupishania na cha nane kinachoanzia Malagarasi -Musongati kitakuwa na urefu kilometa 110, njia kuu kilometa 84 na kilometa 26 njia za kupisha kikiwa kimebuniwa mahususi kwa ajili ya kubeba mizigo mizito na abiria.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisalimiana na Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye wakati wa uzinduzi wa reli ya kisasa SGR Uvinza - Musongati.

Kimsingi huu ni mradi mkubwa wa kwanza kutekeleza kwa ushirikiano wa nchi mbili katika ukanda wa Afrika Mashariki ni kielelezo cha ushirikiano mzuri baina ya nchi hizo.

Waziri Mkuu Majaliwa anasema serikali ya Tanzania na ile ya Burundi zilikubaliana kujenga tawi la reli la Uvinza hadi Musongati kwa lengo la kuunganisha migodi inayopatikana katika maeneo hayo na Bandari ya Dar es Salaam inayosafirisha mizigo mingi katika ukanda huo.

Anasema, "Reli hii itarahisisha usafirishaji wa bidhaa ikiwemo madini ya nikeli, hivyo basi nikeli hii itasafirishwa na reli yetu tuliyonayo, hivyo inakwenda kuchochea mahusiano, biashara na kufungua fursa zaidi kiuchumi."

Hatua hiyo ni moja ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayojielekeza katika kuifanya Tanzania ijiimarishe katika ushirikiano na nchi nyingine za Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika kuhakikisha sera za kikanda zinaakisi na kulinda maslahi ya kiuchumi ya taifa na kuendeleza biashara na uwekezaji.

Majaliwa anasema mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya dira na ajenda ya AU 2063 inayosisitiza kuunganisha nchi za Afrika kupitia miundombinu bora na ya kisasa ili kukuza mshikamano na ustawi wa maendeleo ya wananchi.

"Reli hii ni injini mpya ya uchumi wetu na ni Reli ya kwanza inayounganisha nchi na nchi kikanda," anasema Majaliwa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye wakichanganya udongo kuashiria ushirikiano wa ujenzi wa reli hiyo.

Ujenzi wa reli hii utakuwa wa kipindi cha miaka mitano na mwaka mmoja wa matazamio.

Mradi huo utagharimu Dola za Marekani bilioni 2.1 sawa na Sh trilioni 5.1 na unatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 5,000.

Profesa Mbarawa anataja faida za reli hii pale itakapo kamilika na kuanza kutumika kuwa ni kupungua kwa gharama za usafirishaji mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Bujumbura kwa asilimia 40.

Anasema kwa sasa kusafirisha kasha moja kutoka Tanzania kwenda Burundi ni Dola za Marekani 3,800 (Sh milioni 9.9) lakini reli hii itapunguza na kufikia Dola 2,000 (Sh milioni 5.2) kwa kasha moja.

Aidha reli hiyo itawezesha usafirishaji wa mizigo mingi kwa wakati mmoja ikilinganishwa na ilivyo sasa na kupunguza muda uliokuwa unatumika kusafirisha mizigo.

Kwa sasa sasa safari moja huchukua muda wa saa 96 takribani siku nne hadi tano lakini itakaposafirishwa na reli hii itachukua saa 20 pekee.

Profesa Mbarawa anasema kwa sasa lori moja lina uwezo wa kusafirisha tani 30 lakini reli hiyo ikianza usafirishaji itasafirisha tani 3,800 kwa safari moja.

Reli hiyo pia itatumia nishati ya umeme utakaozalishwa kwa kutumia vyanzo vya asili na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa ambayo ni ajenda ya nchi nyingi duniani.

Kadhalika reli hiyo itawezesha migodi ya nikeli iliyopo Musongati, Burundi kusafirisha madini yake hadi Bandári ya Dar es Salaam na mradi huo utaboresha maisha ya watu.

Profesa Mbarawa anasema mradi huo utakapokamilika utatoa fursa kwa nchi za EAC kufanya biashara na kuimarisha utangamano wa kikanda na kuleta ustawi wa jamii.

Faida nyingine ni kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam kwa kuwa na uwezo wa kuzihudumia nchi zinazotumia bandari hiyo na kuimarisha ushoroba wa kati katika biashara za kikanda.

Reli hiyo pia inatarajiwa kukuza uchumi wa kikanda kwa kuunganisha masoko yaliyopo nchini na yale ya nchi za nje na kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu za usafirishaji katika maeneo hayo na itakuwa kichocheo cha maendeleo ya viwanda, kilimo, sekta ya madini na sekta nyingine za uzalishaji kwa kutoa huduma ya usafiri wa uhakika.

Kwa upande wake Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye, anasema utekelezaji wa mradi huo utatoa fursa mpya za kibiashara na kuimarisha mtangamano wa kikanda.

"Reli hii itafungua fursa mpya za kibiashara, kuongeza ajira, na kuimarisha mshikamano wa kikanda, ni hatua kubwa kuelekea mustakabali wa ustawi wa watu wetu," anasema Ndayishimiye.

Naye Waziri Mkuu wa Burundi, Nestor Ntahontuye anasema reli hiyo italeta mageuzi makubwa katika sekta ya usafirishaji na kufungua milango ya uwekezaji mpya nchini Burundi.

CamScanner